JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI MEI NA JUNI, 2026

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 baadhi ya maeneo ya nchi yaliendelea kupata vipindi vya mvua hususan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hali hii ilisababisha ongezeko la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa baadhi ya maeneo, lakini pia mafuriko na kutuama kwa maji katika maeneo mengine. Katika kipindi cha mwezi Juni, 2026, vipindi vya upepo mkali vilianza kujitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe. Hali hii ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa za mwelekeo wa misimu ya mvua pamoja na Kipupwe zilizotolewa hapo awali.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Mei, 2026


Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vifupi vya mvua kubwa pamoja na ngurumo vilijitokeza katika maeneo machache ya nchi na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali, na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 99.7 kilirekodiwa katika kituo cha Matangatuani (kisiwa cha Pemba) mnamo tarehe 2 Mei, ikifuatiwa na milimita 92.1 katika kituo cha Musoma (mkoa wa Mara) mnamo tarehe 5 Mei pamoja na milimita 69.9 katika kituo cha Lyamungo mnamo tarehe 1 Mei, 2026.

Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 02/2026*





**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Mei, 2026.

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Mei, 2026

Katika kipindi cha mwezi Mei 2026, hakuna ripoti ya vipindi vya joto kali vilivyorekodiwa nchini. Aidha, kiwango cha juu zaidi cha joto cha nyuzi joto 33.2 °C °C kilirekodiwa katika kituo cha Kibaha (mkoa wa Pwani) mnamo tarehe 11 Mei, 2026.

Kwa upande mwingine, hali ya baridi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Kituo cha Uyole kilirekodi kiwango cha chini kabisa cha joto la chini cha nyuzi joto 7 °C tarehe 30 Mei, 2026. Kwa ujumla, Vituo vilivyorekodi viwango vya joto chini ya nyuzi joto 10 vilika Uyole(siku 14 za mwezi) pamoja na Igeri siku 16).
Kielelezo 2 kinaonyesha viwango vya joto la chini katika vituo vya Igeri na Uyole kwa mwezi Mei. Mtawanyiko huu unaonyesha kua vipindi vya baridi vilianza mnamo wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2026.




**Kielelezo 2:** Viwango vya joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Mei, 2026.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Mei, 2026

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa ziwa Viktoria (mikoa ya Shinyanga na Mwanza), kanda ya kati (mikoa ya Singida na Dodoma) pamoja na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Iringa na Songwe).

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Juni, 2026

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2026 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani, ziwa Viktoria, maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na nyanda za juu kusini magharibi. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache. Viwango vikubwa vya mvua kurekodiwa katika kipindi hichi vilikua milimita 55.2 katika kituo cha Matangatuani mnamo tarehe 1 Juni, na milimita 55,0 katika kituo cha uwanja wa ndege cha Zanzibar mnamo tarehe 16 Juni, 2026.

### 1.5 Hali joto kwa mwezi Juni, 2026

Katika kipindi cha mwezi Juni 2026, hakuna vipindi vya joto kali vilivyoripotiwa nchini. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 31.9 °C kilirekodiwa katika kituo kituo kilichopo uwanja wa ndege wa Kigoma mnamo tarehe 16 Juni, 2026.

Kwa upande mwingine, hali ya baridi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nyanda za juu kusini magharibi. Vipindi vya baridi ya wastani hadi baridi kali viliripotiwa na kiwango cha chini zaidi kilikua nyuzi joto 3 °C katika kituo cha Uyole (mkoa wa Mbeya) mnamo tarehe 28 Juni, ikifuatiwa na nyuzi joto 4 °C na 4.1 °C katika kituo hicho cha Uyole kwa tarehe 22 na 29 Juni, 2026.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**


*728G _ 02/2026*

Jedwali namba 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo kituo kimerekodi kiwango cha joto la chini cha nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 °C.

Jedwali 1. Idadi ya siku ambazo vituo vilirekodi viwango vya joto la chini vya nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 katika mwezi Juni, 2026

| Kanda | Kituo | Idadi ya Siku (≤ 10 °C) | Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa (°C) |
|---|---|---|---|
| **Nyanda za juu kusini magharibi** | Uyole | 17 | 3.0 °C |
| | Igeri | 22 | 5.4 °C |
| | Mbozi | 17 | 6.4 °C |
| | Iringa | 3 | 7.5 °C |
| | Sumbawanga | 8 | 7.6 °C |
| **Magharibi** | Mpanda | 2 | 8.9 °C |
| | Tumbi | 3 | 9.8 °C |
| **Kanda ya kusini** | Songea | 1 | 9.1 °C |

Kielelezo cha 3 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku kwa mwezi Juni, 2026 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi ilianza kujitokeza katika wiki ya pili mwezi Juni. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha siku nyingi (takribani siku 22) zenye hali ya baridi zaidi zilijitokeza katika maeneo ya Igeri ukilinganisha na meneo mengine.




**Kielelezo 3**. Viwango vya joto la chini katika vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi June, 2024.

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Juni, 2026**

Kuimarika kidogo kwa migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini ilipelekea kutokea kwa vipindi vya upepo mkali wa kusi unaofikia au kuzidi kilomita 40 katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), kati mwa nchi (Singida), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) na maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza na Shinyanga). Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 13 Julai, 2026*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**